SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 USULI WA TATIZO

Neno *taarab* limefasiriwa na wataalamu mbalimbali na kuweza kutoa maana yenye kukaribiana. Kwa mujibu wa Raisi wa Tanzania Mzee Mwinyi, akinukuu kamusi ya 'Al- Maurid' anasema: " *Taarab ni furaha iliyokithiri, raha iliyoje, starehe, staladhi, tafrija, muziki, kuimba au kughuni*"

Ni dhahiri kuwa, katika maendeleo ya muziki wa taarab hivi sasa, nyimbo za huzuni nazo zimeibuka kila pembe mithili ya uyoga. Hali hii ya nyimbo za furaha na huzuni zimekuwa ni sehemu ya maisha ya mwanadamu. Ongezeko hili la nyimbo za huzuni katika tasnia ya muziki wa taarab haliendani kabisa na dhamira na lengo halisi na asilia la uanzishwaji wa muziki wa taarab. Wakati huo ni kwasababu muziki kwa watawala ndani ya kasiri ya taarab, ulikusudiwa kuwapa furaha na starehe tabaka tawala ikiwa ni sehemu ya burudani wakati wa mapumziko. Haikutarajiwa Sultan awe na huzuni, kwani hupewa kila atakacho. Taarab baada ya kuwa muziki wa makabwela, tanzia na huzuni, haziachi kuwepo katika maisha yao halisi.

1.2 WASIFU MFUPI WA FATMA ISSA JUMA

Fatma Issa Juma ni mwimbaji mtia sauti na mshairi wa taarab asili. Amezaliwa Kianga wilaya ya Magharibi mwezi wa Oktoba mwaka 1957. Fatuma ni mtoto wa pili kati ya watoto wane wa mzee Issa Juma. Aliingizwa katika tasnifu ya taarab na mama yake ambaye naye alikuwa mahiri katika tasnia ya taarab. Hivyo mwaka 1973 mama yake alimpeleka katika kikundi cha Culture Musical Club cha Zanzibar. Hatahivyo, mwaka 1976 aliacha rasmi shughuli za uimbaji na kushughulikia kulea watoto wake. Katika mwaka1977 Fatma alishindwa kujizuia kutoshiriki katika taarb, nakurudi tena Katika uwanja wa taarab. Nyimbo yake ya mwanzo ilikuwa*"Wali mtamu na Muhogo Vilevile'*..

katika mwaka 1985, Fatma alirudi tena Culture. *Alipokuwa na kikundi cha Culture, Fatma* alitunukiwa nyimba kadhaa kuimba jambo

lililowagananya wasanii wenzake wamwonee gere. Nyimbo alizoimba wakati huo zilikuwa *‹Kiwe ›, ‹Mbuzi ›, Maafa‹* nakadhalika,alizopewa kuimba katika Culture ni kama*;‹ Mbuzi ›, Kiwe ›, Maafa‹* nakadhalika.

Joto la husuda na choyo kutoka kwa wasanii wenzake lilimsukuma kutunga nyimbo zake mwenyewe kama, Bugudha sitaki, Haya Maumbile yangu, Kunionya sikatai ‹akadhalika. Nyimbo hizi zilimng‹ arisha sana Fatma Issa hata Kutajwa kuwa miongoni mwa waimbaji bora katika mwambao wa Afrika ya Mashariki. Mbali ya kuwa Culture Fatma Issa alijiunga na vikundi vya taarab vya Jeshini (JKU) kama mkufunzi.

1.3MALENGO YA UTAFITI

1.3.1 LENGO KUU

Utafiti huu ulilenga kuchunguza dhamira za nyimbo za huzunikatika taarab.

1.3.2 MALENGO MAHSUSI

a) Kuorodhesha baadhi ya za nyimbo za waimbaji wate ule.

b) Kubainisha sabhau zilizopelekea kutungwa kuwa hizo, na;

c) Kutathmini jamii ilivyopokea nyimbo hizo za taarab na athari yake.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

a) Nyimbo za huzuni zilizoimbwa na fatma zina dhamira gani?
b) Zipo sababumahasusi zinazopelekea kutungwa kwa nyimbo hizo?
c) Jamii zimezipokeaje dhamira za nyimbo za huzuni za waimbaji hao?

1.5 MANUFAA YA UTAFITI

Tasnifu hii ilitazamiwa kuwa ni chachu ya kuwawezesha wasomaji kujua dhamira na sababu ya kutungwa kwa nyimbo zenye za taarab maudhui ya huzuni katika jamii.pia utafiti huu utaiwezesha jamii kugundua nafasi na mchango wa nyimbo za huzuni katika jamii.aidha, utasaidia kuondosha dhana kuwa nyimbo hizo za taarab ni za furaha na ramsa tu na sivyo vyenginevyo.

1.6 NADHARIA YA UTAFITI

Utafiiti huu umeongozwa na nadharia ya uhalisia.Hivyo, ukusanyaji wa data, uchambuzi nauwasilishaji wa data hizo uliongozwa na nadharia hiyo.Nadharia hii ilizuka baada ya Vita Vikuu vya pili vya Dunia baada ya watu wengi kuathirika na madhara ya vita hivi.Athari hizo ni kama vile umasikini,njaa,vifo,mporomoko wa uchumi nakadhalika. Nadharia hii iliasisiwa na mwanafalsafa Hegel katika miaka ya 1980 ya karneya ishirini. Nadharia hii inawaza kuhusishwa na kazi ya kifasihi za Kiswahili, na inebainisha misingi mikuu miwili anbayo inawaza kutumika katika kuongoza uatafiti huu.Misingi hiyo ni;

a) Msingi wa kimhakiti. Huu ni msingi ambao uanaeleza matukio kama

yalivyo katika maisha ya kila siku bila ya kubadilisha kitu hata kimoja.

b)Msingi wa ushabihi ukweli. Huu ni msingi ambao unakaribia kueleza matukio kama yalivyo bila ya kuongeza au kupunguza.

SURA YA PILI

USANIFU NA MBINU ZA KUKUSANYIA DATA

2.1 ENEO LA UTAFITI

Utafiti huu ulifanyika katika kisiwa cha Unguja katika Wilaya ya mjini na viunga vyake. Maneno haya yaliteuliwa kwa kuangalia vigezo thabiti ambavyo upatikanaji wa data utakuwa ni rahisi. Katika sehemu hizi wapo wadau na wapenzi wa muziki wa taarab ambao kwa kiasi kikubwa wanafuatilia kwa karibu sana nyimbo za Shakila na Fatma.

2.2 UKUSANYAJI WA DATA

Kipengele hiki kinaelezea njia na zana mbalimbali ambazo zitakazotumika katika ukusanyaji wa data.

2.3 USAILI

Mtafiti alitumia mbinu ya usaili kwa washabiki na wapenzi wa muziki wa taarab hususan nyimbo za Fatma Issa na hata kwa watangazaji wa vipindi vya taarab asili katika redio. Mtafiti alitumia njia hii ili kupata taarifa hata kwa wale wote ambao hawajui kusoma na kuandika. Kwa upande wa watangazaji wa redio mbinu hii ilimsaidia mtafiti kubadilishana mawazo ana kwa ana ili kupata taarifa za undani kuhusiana na taarab asili.

2.4 USHUHUDIAJI

Mtafiti alitumia mbinu hii kwa kushiriki baadhi ya maonesho ambayo yalitendeka katika majukwaa mbalimbali ili kuona jinsi gani nyimbo hizo zinavyoathiri au kuteka nyoyo za watu.

2.5 ZANA ZA KUKUSANYIA DATA

Mtafiti atatumia zana tofauti ili kukamilisha utafiti.

Zana hizo ni kama :

2.5.1 KAMERA

Kamera itatumiwa na mtafiti kupiga picha sehemu ambazo zitaonesha waimbaji na waimbaji na waimbaji wakiwa jukwaani. Pia itatumika picha kupiga nao waimbaji hawa wateule na makundi mengine ya watafitiwa.

2.5.2 SIMU

Mtafiti atatumia simu kwa ajili ya mawasiliano ukusanyaji wa data na kwa ajili ya mawasiliano,pili,ni kwa ajili ya kurekodi na kupiga picha ikiwa haja imetokea.

2.5.3 DAFTARI NA KALAMU

Mtafiti atatumia daftari na kalamu katika ukusanyaji wa data ili kuandika taarifa muhimu zinazohusiana na utafiti na kutunza kumbukumbu mumhimu katika kwa wasailiwa.

2.5.4 NGAMIZI

Mtafiti atatumia ngamizi katika kuchapa na kuangalia baadhi ya taarifa katika tovoti mbali mbali.

2.6 USALITI WA RAFIKI AU NDUGU

Usaliti kati ya rafiki, ndugu au jamaa lipo katika jamii zetu yule mtu wa karibu ambaye anamuweka kama ndugu yake humfanyiya vitendo amb avyo havistahiki kufanyia ndugu au rafiki yake wa ukwali.Iingawa katika jamii jambo hili hujitokeza mara kwa mara katika hali halisi ya maisha ya mwanadamu. Utafiti huu umebaini kuwa ndoa nyingi huvunjika kutokana na mikataba ya kbiashara na mengine na usaliti ulokithiri.

Hivyo,wasanii hutunga nyimbo za huzuni kwa lengo la kuonesha utumbo uliopo katika jamii hizo.Kutokana na hali hiyo nadharia ya uhalisia inakwenda sambamba na matukio yanayotokea kama yalivyo katika jamii kutokana na usawiri wa hali halisi ya maisha ya mwanadamu.

SURA YA TATU

UCHAMBUZI NA MATOKEO YA UTAFITI

3.1 DHANA YA HUZUNI

Huzuni kwa mwanadamu ni ile hali ya masikitiko, majonzi, jitimai au simanzi ambayo mtu huipata ndani ya nafsi yake. Huzuni huwa na visababishi kadhaa katika jamii. Hali hizo ni kama vile masiba, maradhi, usaliti na kadhalika. Dhana ya huzuni katika maisha mwanadamu si ngeni masikioni mwa walio wengi, kwani hali hii hujitokeza mara kwa mara katika maisha halisi ya kila siku. Mwanadamu hupata na huzuni kupitia mambo mbalimbali yanayotendwa. Huzuni humfika mtu yoyote lakini kila mtu huwa na namna yake ya kuipokea au kuikabili. Mwengine humfika akanyamazas asitake mwengine ajue.Huweza mtu kumpata akasononeka nayo na kumuathiri. Wale wachache wenye vipaji wakiwemo washairi na waimbaji hawaifutiki huzuni, huitoa hadharani wakati mwengine bila sababu.

3.2 MSIBA

Msiba ni ile hali ya mtu kuondokewa na mwenza wako au mtu wake wakaribu sana.Hali hii ikijitokeza mwanadamu hawezi kuzuia. Mungu huwa tayari ameshalipanga limtokezee mja wake.Mtu baada ya kuondokewa na mbendwa wake kwa kusafiri au kuaga dunia hapo ndipo moyo hujawa na huzuni na simanzi ambazo ni vigumu kusahau.Wimbo waAdui kiumbe. Ulioimbwa na Fatma Issa unabainishanmasikitiko hayo kwa binadamu wenzake.

3.4 MALIWAZO NA UFARIJI

Imebainika kuwa wasikilizaji wanapozisikiliza nyimbo za taarab asiliazenye maudhui ua huzuni na majonzi nao wao huguswa kwa hisia nzito zutokana na kukumbuka hali ambauo hata wao imewakuta mmoja ya washabiki wa nyimbo hizi na mwimbaji Fatma anasema, napozisikia nyimbo za huzuni hukumbuka mambo anbayo yanayowasibu watu kadhaa katika jamii yake.Anaposikiliza nyimbo hizo wakati mwengine hujikuta anatokwa na

Liliomponza kule kumumini bila ya kiasi na kuacha kumchunguza.Malipo yake ni kumuhasidi na kumfitini.

3.4 HUZUNI NA KUMBUKUMBU

Utafiti huu umebaini kuwa, wapo baadhi ya watu ambao walisikiliza nyimbo hizi za huzuni hapo zamani na bila ya kutambua nyimbo hizi zina mchango katika jamii. Watu hawa walikuwa wamezoweya kusikiliza nyimbo za furaha pekee. Hii ni kwasababu na kuwa jambo ambalo linazungumziwa la huzuni huwa halijamgusa bali akisikiliza nyimbo kwa lengo la kujiburudisha tu. Bwana Ali wa skuli ya Nyuki [2]anasema kuwa hapo zamani nyimbo za huzuni alikuwa hazitilii manani sana kwasbabu alikuwa anamwona mwimbaji ni mtu mwenye kusikitikatu tu kwa hiyo hapo hakuona faida yoyote ya hizi nyimbo. Lakini kwa kadri siku zilivyoendelea kusonga mbele nay eye binafsi kuyakabili matatizo mbalimbali katika jamii ndipo anapojenga taswira kuwa kumbe nyimbo hizi zilikuwa zikionesha hali halisi ya misha ya mwanadamu. Akitolea mfano nyimbo ya **Asokasoro Hakuna** ni wimbo ambao umeimbwa zamani lakini kwasasa ndiyo wimbo anauelewa lengo na dhamira yake katika jamii. Hivyo, kutokana na hali hiyo mtafiti amebaini kuwa nyimbo za huzuni huweka kumbukumbu akilini mwa msikilizaji. Kwani hukumbuka kuwa zamani ziliwahi kuimbwa nyimbo za huzuni ambazo kwa namna moja ama nyengine huburudisha na kuelimisha jamii. **Asokasoro** ni wimbo uliotungwa na kuimbwa na Fatma ambao mashairi yake humkumbusha Ali vitu vingi ambavyo hapo awali hakuvitambua. Baadhi ya beti zinzsema hivi;

Wala sini vibaya *mimi kunielekeza*
Kinachonipa udhia *ni kule kuniapiza*
Asokasoro Hakuna *aloumbwa na muweza*
Mwaenye lile hili hana *ndio shani yake azza*
Tabia kutolingana *sijambo la kushangaza*
Kinachonikera sana *nisonalo kupakaza*

Kunisema sichukui
Kusengenya haifai
Ni hekima njema rai

Wimbo huu anapousikiliza humkumbusha mbali sana kwa kuwajuwa walimwengu walivyokuwa na tabia ya kusengenyana na kupakaza uovu ambao hata haupo skatika ulimwengu huu. Hivyo, mwimbaji anadhihirisha huzuni zake kwa kusema kuwa si jambo jema kukaa na kuanza kumsengenya na kumsema jambo la msingi ni kukaa na kumuita na kumuouya kwa mambo yote ambayo mja anahisi kuwa si mazuri na hiyo ndiyo itakuwa ni njema rai.

3.5 HUZUNI NA MAJUTO

Mwimbaji Fatma kwasababu ya dunia ameamua atuliye, katika numbo nyengine anaonesha majuto yake kwa mpenzi wake ambae alimthamthamini na kumsabilia hapo awali kila kitu katika maisha yake kwa mpenzi wake ambae alimthamini na kumsabilia hapo awali kila kitu katika maisha. Mpenzi wake huyo alikuwa akibadilisha wanawake wa kila aina. Ndipo hapo aliposhindwa kuvumilia akaamua atunge na aimbe yeye mwenyewe nyimbo ya ***Nenda Utakapo.*** Wimbo huu unaonyesha jinsi ya mume asivyothamini mapenzi ya mke ambaye anampenda. Anaimba hivi;

Unavuma mja wavuma ***kipanga*** wallahi sikukutambuwa
Unayataka sikupinga *maridhiya nilikuwa*
Kama ***mboni ya macho*** *nnavyokuenga* *mamlaka nilikuwa*
Kumbe vile ni ***mjinga*** *hujui kuthaminiwa*

3.6 HUZUNI NA BAHATI

ndipo yeye aiipojiaminisha kuwa yeye hana bahati ya kupendwa na wasanii wenzake. Yeye anaamini kinachompnza ni kipaji chake cha kuimba. Hali hii ndiyo inayompa hamu na shauku ya kutunga nyimbo nyingi yeye mwenyewe binafsi.

Yawezekana ukosefu wa bahati kama upo kwa watu wengine. Yeye hili limepalilia kipaji chake. Wimbo wa Sijali Kuchukiwa, uliotungwa nay eye Fatma anavyochukiwa na watribu wenzake. Ingawa yeye anajitahidi kukaa nao kwa wema na hisani, haiwi nusura kwake ya kupata bahati. Fatma analalama;

Sitoyalipiza katu *hauo unayonitendea*
Kuvumiliya si kitu *mitihanai ya duniya*
Ninange kwa kila mtu *na ubaya kunitiya*

Kitachokulipa ni utu *uovu sitokufanyia*
Kinyume siendi siendi kuntu *hata ukinishukiya*
Rohoni mwangu siweki kitu *japo nishayazoeya*

Kama nimekukosea *mie yailahi ndiye hakimu*
Na kama unanioneya *ni yeye atohukumu*
Hukumu hukumu *hakimu hukumu*

Ongeza kunifisidi *kwa kisa na kila mambo*
Tukana niite hasidi *ukioniona vikumbo*
Kustahmili nazidisubira *ndo zangu nyimbo*

Japo wanikera hadi *sitokujibu kwa fumbo*
Madhali Mungu shahidi *kwako siongezi jambo*
Hakimu wa haki wadudi *yatakwisha majigambo*

3.6 KUREKEBIKA TABIA

Kupitia nyimbo za huzuni jamii inapata manufaa makubwa kutokana na kuwa nyimbo hizi huirekebisha jamii kwa kuona chimbuko, athari na matokeo yake kupitia masuala mbalimbali. Nyimbo huweza kuifanya jamii ibadilike na kuachana na mambo ambayo hayapaswi kufanywa na mwanadamu. Nyimbo hizi hukemea ufisadi na mambo mengi yakiwemo choyo na maovu mengine. Mfano wa nyimbo za huzuni ambazo zinashajiisha watu kutoo neana choyo nag ere bali mtu afanye bidii ili aweze kufanikiwa ni kama vile; Haya maumbile YangunaAsokasoro Hakunazilizotungwa na kuimbwa na Fatma. Nyimbo hizi zinakataza tabia ya husuda na kuoneana maya na kumtaka mtu atafute njia mbadala ambayo itemwezesha kufanikiwa katika maisha yake. Bia, kupitia wimbowa Mapenzi Yamepunguaulioimbwa na kutungwa na Shakila, mwimbaji anawasihi

wawili wapendanao wawe na mapenzi ya kweli ili waweze kupiga hatua za kimaendeleo katika jamii. Wasia unaotoiewa in si busara wala si hekima mpenzi mmoja kumdanganya mpenzi mwingine.

MAREJEO

Andanega A.A.S (2002)" *Bahari ya Elimu ya Ushairi* ". Ndanda Mission Press, Mtwara.

Alawiy, Z. (2007) " *Nyimbo za Mafumbo za Taarab zinavyochangia kudumisha maadili ya jamii ya wazanzibari*" , Ripoti ya utafiti kwa ajili ya shahada chuo kikuu Suza, (haijachapishwa).

Alhabib, E.A (2012) " *Matumizi ya lugha katika Nyimbo za Taarabu* " Tasnifu ya Umahiri katika Kiswahili, Chuo kikuu Huria Tanzania.

Babbie, E (1992) *The Practice of Social Research*. 6th edition. Wadsworth Publishing Company.

Best and Kahn, J. (1993). *Research in Education*. New York: Allyn Bacon Inc.

Cohen, L, Manion, L and Morrison, K (2000) *Research Methods in Education*. 5th edition. London: Rutledge Falmer.

Jilala, H. (2008) The Artistic Uses of Metaphor in Constructing Meanings and Messages in New Generation Songs in Tanzania. MA Dissertation,(Unpublished) University of Dar es Salaam.

Kahigi K.K. (1995). *Lugha Katika Vitabu Vya Watoto.* Katika Kahigi K.K. (mh), Kioo cha lugha: Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juzuu, Na. 1. (uk. 21-36).

Kombo, D.K. and Tromp, D. L.A, (2006), *Proposal and Thesis Writing: Intoduction*, Kenya, Paulines Publications Africa.

Kothari, C. K (1990) *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C.R. (1993). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C. R. (2001). *Research Methodology: Methods and Techniques*. Ed. New Delhi: Wiley Eastern.

Kothari,R.C. (2004) *Research Methodology. Methods and Techniques* New Delhi:

New Age International (P) Limited, Publishers.

Lakoff, G. and Johnson, M. (1980). *Metaphor We Live By*. Chicago: University of Chicago Press.

Lakoff, G. and Turner, M. (1989) *More Than Cool Reasons. A Field Guide to Poetic Metaphor*. Chicago: University of Chicago Press.